

# Ufuatiliaji Baada ya Mkutano wa Elimu Inayomlenga Mtoto (IEP)

Ufuatiliaji wa mzazi baada ya mkutano wa IEP utahakikisha utekelezaji wenye fanaka wa IEP kwa mtoto. Yafuatayo ni baadhi ya mapendekezo:

- Fuatilia maendelo ya mtoto wako. Fahamu ni mara ngapi ripoti ya maendeleo na mawasiliano kutoka shuleni vitafanyika lakini kumbuka unaweza kufuatilia shuleni na uombe kujua hali ya mtoto wako wakati wowote.
- Omba kufanywe mkutano kama maendeleo hayajaridhisha au kama matatizo ambayo unaamini huenda yanaathiri mtoto wako yameanza kujitokeza.
- Tarajia uhakiki wa mwisho wa mwaka/au ikipungua mkutano na timu ya shule kutathmini hali ya sasa mtoto wako.
- Hakiki hali ya mtoto wako kabla ya kipindi cha mpito (i. E. shule ya msingi kwenda ya kati.) Tafuta kujua ni kipi kilienda vizuri na ni kipi kinafaa kuwepo kwenye IEP inayofuata.
- Elezea shukurani zako kwa kazi wanayofanya walimu. Wacha wajue ni kipi kinaenda vizuri. Wacha wasimamizi wao wajue pia.



**Kumbuka IDEA 2004 inahitaji kwamba IEP ieleze ni lini ripoti za mara kwa mara kwa wazazi kuhusu hatua wanazoendelea kupiga watoto kuelekea kufikia malengo ya kila mwaka zitatolewa.**

## Fuatilia hatua za maendeleo ya mtoto wako.




Baada ya IEP kuandikwa na mara utekelezaji wa IEP unapoanza, ufuatiliaji wa IEP unafaa kufanyika. Ufuatiliaji ni mchakato unawahusisha wazazi, watoa huduma, walimu, na wengine wanaohusishwa na mtoto ili kutathmini mara kwa mara jinsi programu ya mtoto inavyofanya kazi. Ufuatiliaji ni muhimu sana kwa sababu huwezi kujua kwa hakika kama programu au lengo litafanyika kwa mtoto. Kama

utawahi tatizo mapema, utakuwa katika nafasi nzuri ya kusuluhisha na timu kwa muda mzuri ili kufanya mageuzi yanayohitajika kwenye programu.

**Kama mzazi, una uhuru wa kuamua kama ungependa kupokea au kutoa maoni ya mara nyingi juu ya utendaji na ukuaji wa mtoto.**

### **Baadhi ya Mbinu za Kufuatilia Programu ya Mtoto Wako:**

- Tathmini ripoti ya maendeleo. Ripoti ya maendeleo inafaa iweke rekodi ya kuonyesha ni hatua gani nzuri mtoto wako anapiga katika eneo fulani.



- Tumia muhtasari wa nyumbani wa kila siku au kila wiki kwa ajili ya mtoto wako. Muhtasari wa nyumbani unaweza kufa daftari ambalo linaenda nyumbani kila wakati kuhusu mtoto wako, au vipengele maalumu vinavyoangaliwa kwenda na kurudi.
- Weka “faili ya nyumbani” ya sampuli ya kazi za mtoto wako, maandishi ya mwalimu na mawasiliano, nakala za IEPs, nakala za matokeo ya tathmini, n.k.
- Andika sifa kuhusu maendeleo au ugumu mtoto wako jinsi unavyoona akiwa nyumbani.
- Angalia kazi anayokuja nayo nyumbani mtoto wako. Kama kazi ni chwarachwara kila wakati, haijakamilika au ina majibu yasiyo sahihi, hiyo ni dalili ya tatizo. Kama kazi ya mtoto wako haiongezi kwa ugumu, hiyo ni dalili ya tatizo. Aidha, tambua kama kazi inampa au haimupi changamoto ya kutosha mtoto wako.
- Amini silika yako. Kama mtoto wako anaonekana asiye na furaha au ni mgonjwa au ‘unahisi’ kuna jambo baya, unaweza kuitisha kikao na mwalimu.
- Kutumia barua pepe ni njia faavu sana ya kuwafahamisha wanachama wote wa timu ya IPE kwa wakati mmoja kuhusu mahitaji ya mwanafunzi. Inakupa njia faavu ya kujifahamisha wakati wote kuhusu maendeleo ya mtoto wako huku ukiendela kuweka rekodi ya maingiliano yako na wanachama wa timu ya IEP.

Maudhui haya yametolewa katika kitabu cha Utah Parent Center handbook:

Kijitabu cha Parents as Partners in the IEP Process Parent Handbook



Utah Parent Center